

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

USAJILI WA MABASI YA DALADALA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

Kutokana na malalamiko ambayo Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) imekuwa ikipokea kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu upatikanaji wa huduma za usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam, Mamlaka ya SUMATRA iliamua kufanya uchunguzi na kubaini kuwa baadhi ya mabasi yaliyopewa leseni ya usafirishaji abiria Jijini Dar Es Salaam hayatoi huduma hiyo kwa mujibu wa leseni zao na hivyo kusababisha utoaji wa huduma ya usafiri wa umma kutotosheleza mahitaji ya wakazi wa Jiji.

Kutokana na hali hiyo Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) imechukua hatua zifuatazo:

1. Kuendelea kutoa leseni ya usafirishaji abiria kwa njia zote za Jiji.
2. Kuhimiza wamiliki wa mabasi ambao hawakuendeleza leseni za mabasi yao katika baadhi ya njia kutokana na sababu mbalimbali kufika katika ofisi za SUMATRA kwa ajili ya kuendeleza leseni hizo.
3. Kupokea maombi kutoka kwa wamiliki wa mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria 25 na kuendelea kuwasilisha maombi ya leseni ya usafirishaji ili waweze kutoa huduma hiyo kwa mujibu wa Sheria na taratibu za utoaji huduma ya usafiri wa umma.

Ni matarajio ya SUMATRA kuwa wamiliki wa mabasi ya abiria watatoa ushirikiano kwa kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa mabasi yao wanafuata Sheria na kuacha vitendo vya kihalifu kama kukata ruti, kuiba ruti, kutoza nauli kubwa na vitendo vingine vyote vinavyosababisha usumbufu kwa abiria.

Aidha watumiaji wa huduma za usafiri na wananchi kwa ujumla wanaombwa kuendelea kushirikiana na Mamlaka ya SUMATRA kwa kutoa taarifa kila wanapobaini mtoa huduma anakiuka masharti ya leseni.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na SUMATRA kupitia namba ya simu 2197500/1, +255783 223013, +255755660016, +255767250550 au tuma barua pepe kwa infor@sumatra.or.tz.

Imetolewa na:

KAIMU MKURUGENZI MKUU

Juni, 2013